

Swahili transcript:

Baraka: Kuhusu matumizi ya lugha, labda mimi naona kuna sababu mbili. moja ni kwa sababu ya ule mseto wa lugha, kwamba mtaala wetu ni wa lugha ya kiingereza. Lakini ukiangalia hata katika ngazi ya chuo kikuu, Kiswahili bado kinatumika sana katika kufundishia, yaani ni masomo ya kiingereza yanafundishwa kwa Kiswahili. Kwa hiyo unakuta sasa matumizi ya hizi lugha mbili yapo sambamba, kwamba katika mazungumzo na katika ufundishaji kinatumika Kiswahili, katika kujisomea binafsi tunasoma kwa kiingereza. Kwa hiyo sasa kwa sababu hiyo unakuta hata mnapofanya mijadala ya kimasomo, mnajaribu kukitoa kile kiingereza na kukifafanua kwa Kiswahili. Sasa hii inapelekea muingiliano mkubwa sana wa lugha kwa sababu ya utofauti wa lugha zinazotumika kufundishia. Kwamba ukiangalia hata walimu wetu madarasani, ni kiingereza sawa lakini wanatufundisha katika mtindo wa Kiswahili. Hata maprofesa chuo kikuu wanafundisha sawa lakini wanatoa ufafanuzi kwa Kiswahili. Kwa hiyo muingiliano wa hizi lugha mbili kama zote kufundishia licha ya kwamba rasmi ni kiingereza ndio inapelekea mchanganyiko mkubwa wa lugha. Lakini vilevile pia ni kama kasumba tu pia watu wengine wamekuwa nayo kwamba ili kuonekana mbele ya jamii kwamba yeye ni msomi, basi lazima anapozungumza aambatanishe na maneno Fulani ya kiingereza kuonekana kwamba ana uelewa mpana. Sasa hii nayo wakati mwingine imekuwa ikimpelekea mtu anajizoeza hivyo mpaka inafika hatua inakuwa ni tabia yake. Lakini sababu kubwa nafikiri ni hii ya kuchanganya hizi lugha mbili katika kufundisha.

Nicholaus: Sawasawa, basi sina maswali mengine, kama labda mna la nyongeza? kama hamna, nashukuru kwa muda wenu.

Mtoa mada: Sisi tunakutakia kazi njema tu na masomo mema, tupo, ukipata tena fursa siku nyingine kuja kutembelea shule yetu na ni shule yako pia, itakuwa vizuri; lakini tunakutakia kwanza safari njema na masomo mema.

Nicholaus:Sawa, asanteni sana!

Baraka: Tunashukuru sana!

Nicholau: Asante!

English translation:

Baraka: What I see is that there are two reasons why people mix Swahili and English as they talk. One is because our curriculum is in the English language. But even at the university level, Swahili is used in classrooms when teaching. I mean subjects are in English, but Swahili is used to clarify while teaching. So these two languages are used interchangeably, during normal conversations and during instruction. Even during discussion, there is a tendency to translate English to Swahili in order to get a clearer understanding of the subject. Teachers, even professors at the university, use two languages when teaching. They teach their subjects in English, but they give clarifications in Swahili. So, using two languages interchangeably in classrooms has caused many people to code-mix Swahili and English. Sometimes, in our society, it is the habit of some people to show that they are educated. When they speak, they must use some English words to show that they have a broad understanding. However, the big reason is that we use two languages at the same time in instruction.

Nicholas: All right. I don't have any more questions. Maybe if you have anything to add..... If not, thank you for your time.

Baraka: We wish you a good journey and good luck in your studies. Whenever you get time, come and visit us in our school. It is your school too. It will be good, but first, we wish you a good journey and good luck in your studies.

Nicholas: Okay. Thank you so much!

Baraka: You're welcome!

Nicholas: Thanks!

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated